

BARAZA JIPYA LA WAFANYAKAZI WA TUME YA TAIFA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA (COSTECH) LAZINDULIWA



Picha ya pamoja ya Menejimenti na Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi la Tume Ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia COSTECH Katika Uzinduzi wa Baraza Jipya uliofanyika Julai 17, 2020 Katika Ukumbi Mkubwa wa Mikutano wa Tume, Dar es Salaam

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia siku ya Ijumaa tarehe 17 Julai imezindua Baraza jipya la wafanyakazi litakalodumu kwa kipindi cha miaka mitatu (2020 mpaka 2023) katika Ukumbi Mkubwa wa Mikutano ulipo Makao Makuu, Kinondoni Dar es salaam.

Akizindua Baraza hilo, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Dkt. Amos M. Nungu aliwashukuru wajumbe kwa kuwapongeza na kulisitiza Sekretarieti kufanya kazi kwa weledi mkubwa na kuhakikisha vikao vya Baraza la wafanyakazi yanafanyika kwa wakati kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Taasisi Bibi. Anna G. Ngoo aliwakaribisha wajumbe na kushukuru uendeshaji wa mchakato wa kuwapata wawakilishi wa Baraza jipya, ulizingatia misingi ya demokrasia uwazi na uhuru wa kila Idara kupata mjumbe mmoja mwakilishi na hatimae kuchaguliwa na amewatakia kila la heri katika kusimamia maslahi ya watumishi.

Wajumbe wapya waliochaguliwa ni Bestina Daniel (Kurugenzi ya Uratibu na Uendelezaji Utafiti), Dkt Andrew Aloyce (Kurugenzi ya Kituo cha Uendelezwaji na uhawilishaji wa Teknolojia), Beatrice Koda (Kurugenzi ya Huduma za Taasisi), Merchades M. Rutechura (Kurugenzi ya Menejimenti ya Maarifa), Said Majid (Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani), Charles Mwabulambo (Kitengo cha Ugavi na Manunuzi), Sia Emmanuel Mlay (Kitengo cha Huduma za Sheria) na Selina Mchao (Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia).

Uchaguzi wa viongozi wa Baraza kwa mwaka (2020 -2023) uliendeshwa na Ndg. Mecky Humbo (*Katibu Kanda ya Mashariki- Chama cha RAAWU*) na Ndg. Deusdedith N. Mshelela (*Mwakilishi wa Kamishna wa Kazi- Ofisi ya Waziri Mkuu -Dodoma*) na kutangaza viongozi wapya Bi. Nichiza Malaki (*Katibu wa Baraza*), Mashuhuri Mwinyihamisi (*Naibu Katibu wa Baraza*) na Bestina Daniel (*Mwakilishi wa Wafanyakazi katika Kamati ya Utendaji*).

Aidha, Mkutano huu uliratibiwa Mwajiri, wajumbe wa **RAAWU (Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu Ya Juu, Utafiti, Sayansi, Teknolojia, Habari Na Ushauri)** wa Tawi la ndani na Bi. Sarah Kabigi (*Mwenyekiti Tawi la COSTECH*) akishirikiana na Katibu wa Kanda walimkabidhi Mkurugenzi Mkuu Mkatiba wa Baraza la Wafanyakazi na Mwenyekiti alizindua Baraza rasmi.

Ndugu. Deusdedith N. Mshelela akitoa mada kwa wajumbe alisitiza umuhimu wa Ushirikishwaji wa wafanyakazi na kuzingatia maslahi ya watumishi kwa lengo la kuondoa migogoro katika sehemu za kazi na kisha

Mwenyekiti alihitimisha Baraza kwa kuwashukuru watoa mada kwa ushiriki wao na kuwakaribisha rasmi wajumbe wapya waliochaguliwa kama wawakilishi wapya katika Baraza la wafanyakazi huku akisisitiza uongozi wa RAAWU Tawi la COSTECH kuhamasisha wafanyakazi kujiunga na chama hicho.

Imetolewa na

OFISI YA UHUSIANO- COSTECH